SERA NA TARATIBU ZA SHIRIKA LA SO THEY CAN

**SERA NA. G012: SERA YA KUZUIA UTAKATISHAJI FEDHA NA UGAIDI**

Mhusika: MKURUGENZI MKUU TOLEO: 2.1

Imeidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi: Tarehe 3 Machi 2021 Tarehe ya Kufanyiwa Mapitio: Machi 2023

**DIBAJI**

Sera hii iliandikwa na Shirika la *So They Can* (International) lililopo Australia kwa ajili ya kutumika katika ofisi zote za *So They Can.* Shirika la *So They Can* lina ofisi tano zilizosajiliwa katika nchi ya Australia, Kenya, Tanzania, New Zealand na Marekani, ambazo ni sehemu ya *So They Can Global Alliance*. Katika sera hii "Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa *So They Can (International*). Isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo "Bodi" maana yake ni bodi ya *So They Can (International*). Sera hii inawalenga wafanyakazi wote wa *So They Can,* Wajumbe wa Bodi na wafanyakazi wakujitolea katika ofisi zote 5 za *So They Can*. Taratibu za *So They Can* zinaendana na sera za *So They Can.*

**UTANGULIZI**

So They Can linapinga aina zote za ugaidi na shughuli za uhalifu. So They Can kwa namna yoyote halitaunga mkono, kuvumilia au kuhamasisha utakatishaji wa fedha, ugaidi na shughuli zozote za wale wanaojihusisha na shughuli za uhalifu ikijumuisha utakatishaji fedha na ugaidi na itafanya jitihada zozote za kuhakikisha kwamba rasilimali hazitumiki kuwezesha shughuli za kigaidi na utakatishaji fedha.

Sera huu inaweka masharti ya So They Can kufuata sheria za Australia zinazohusu kupinga ugaidi na shughuli za uhalifu, kupitia taratibu na sera ambazo zinapunguza hatari ya kuunga mkono magaidi, taasisi zinazojishughulisha na Ugaidi hususani zile zilizo katika Orodha ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na Orodha ya Serikali ya Australia ya Mashirika yanayojihusisha na Ugaidi. Sera hii inashughulikia hatari ya kujihusisha na mashirika au watu wanaojihusisha na uhalifu.

Serikali ya Australia imetunga sheria inayoendana na mikataba kadhaa ya kimataifa ya kupinga ugaidi iliyoandaliwa kwa ajili ya kuzuia ugaidi. Sheria zinazohusika zinazozuia shughuli za ugaidi zinaweza kupatikana katika:

Sehemu ya 5.3 ya Sheria ya Makosa ya Jinai ya Mwaka 1995;

Sehemu ya 10.2 ya Sheria ya Makosa ya Jinai ya Mwaka 1995 ('Makosa ya jinai') na

Sehemu ya 4 ya Sheria ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa ya mwaka ('Sheria ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa')

Sheria ya Makosa ya Jinai inatoa adhabu kali ikijumuisha miongoni mwa mambo mengine kwa upataji fedha kwa kukusudia au bila kukusudia kwa ajili ya shughuli za ugaidi au kupokea pesa kutoka kwa shirika linalojishughulisha na ugaidi (sehemu ya 102.6), kutoa msaada kwa mashirika ya kigaidi (sehemu ya 102.7) na ufadhili wa shughli za kigaidi (103.1). Sheria ya Makosa ya Jinai inabainisha makosa yanayohusiana na utakatishaji fedha (sejemu ya 10.2). Orodha ya mashirika yanayojihusisha na ugaidi kwa madhumuni ya

Sheria ya Makosa ya Jinai yanapatikana katika tovuti ya Ulinzi wa Taifa ya Australia https://www.nationalsecurity.gov.au/what-australia-is doing/terrorist-organisations/listed-terrorist-organisations.

Chini ya Sheria ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa, ni kosa kutoa rasilimali yoyote moja kwa moja au siyo moja kwa moja kwa mtu au taasisi zilizopigwa marufuku. Raslimali kwa ujumla imefasiliwa kama " rasilimali ya aina yoyote, au mali ya aina yoyote iwe ya kushikika au isiyo ya kusikika, ya kuhamishika au isiyo ya kuhamishika" Ingawa Sheria ya Mkataba wa UN ina adhabu chache, kwa upande mwingine ina jumuisha maana pana ya msaada kulingana na muktadha kutokana na fasili yake pana ya rasilimali:

http://dfat.gov.au/international-relations/security/sanctions/Pages/consolidated-list.aspx

Pia, So They Can pia litahakiki orodha mbili zifuatazo ili kuhakikisha halijihusishi na mashirika yoyote ya magaidi na/au watu au taasisi zilizopigwa marufuku.

- Orodha ya Benki ya Dunia ya Kampuni na watu wasiostahiki (Bank Listing of ineligible firms and individuals);

- Orodha ya kampuni na watu waliowekewa vikwazo na Benki ya Maendeleo Asia (Asian Development Bank Sanctions List);

**FASILI**

**Wawakilishi wa So They Can**– ni watu na taasisi ambazo zinafanya kazi kwa niaba ya So They Can bila kujali kama kuna mkataba rasmi wa kisheria au la kati yao na So They Can. Hii inajumuisha lakini bila kikomo wadhamini wote, wajumbe, wakurugenzi, wenye mikataba, washauri waelekezi, wasambazaji, washauri, watu wanaojitolea na washirika wa utekelezaji bila kujali majukumu waliyopewa na nchi zao. Katika nyaraka hii So They Can inajumuisha taasisi yoyote au zote za So They Can zilizosajiliwa Australia, New Zealand, Kenya, Tanzania na Marekani.

**Wahusika** ni wale wanaohusika na usimamizi wa msaada. Kwa ujumla, Wahusika wa Msaada ni bodi, wajumbe wa kamati au wadhamini (ikijumuisha wadhamini au wasimamizi wa ufilisi).

Chini ya kifungu kinachohusu "kuchukua hatua stahiki" So They Can ina wajibu wa kisheria hususani wa kuhakikisha:

a) inawajua watu/mashirika ambayo inayasaidia moja kwa moja;
b) inahakikisha kwamba watu/ mashirika inayoyasaidia moja kwa moja hayapo katika orodha zilizotajwa hapo juu kabla ya kuyapa msaada; na
c) inahakikisha kwamba watu/mashirika yanayopewa msaaada wa moja kwa moja yanafahamu na kuzingatia sheria hizi.

**Utakatishaji Fedha** – ni mchakato wa kuficha chanzo, umiliki au makusudio ya fedha zilizopatikana kwa njia haramu au ya udanganyifu kwa kuziingiza katika shughuli halali za kiuchumi ili kuzifanya zionekane ni halali.

**Kufadhili Ugaidi** –ni kutoa kwa kudhamiria au kukusanya fedha na kutokujali ikiwa fedha zitatumika

kuwezesha au kuhusishwa na vitendo vya kigaidi.

**Kudhibiti Ugaidi** –ni taratibu, mbinu na mikakati inayotumika kuzuia na kudhibiti ugaidi

**SERA**

1. Sheria ya Australia inazuia kujihusisha na watu au mashirika yanayojishughulisha na shughuli za uhalifu, mashirika yanayojishughulisha na ugaidi na/au watu au taasisi zilizopigwa marufuku. Wakati wote So They Can itachukua hatua zenye lengo la kuwezesha kufuata sheria hii.
2. So They Can itahakikisha inatambua sifa na mwenendo mzuri wa watu na mashirika inayoyasaidia na itahakikisha kwamba watu na mashirika hayo si miongoni mwa yale yaliyoorodheshwa na Serikali ya Australia.
3. So They Can will itafanya jitihada zake zote kuhakikisha kwamba shughuli zote (ikijumuisha zile zinazofanywa na washirika au mashirika inayoshirikiana nayo katika kutoa msaada) zinazingatia sheria na kanuni za Australia (na sheria na kanuni za nchi zinazopokea misaada hiyo) ikijumuisha lakini bila kikomo:
    a. Kwa sheria na kanuni zinazohusiana na uzuiaji wa moja kwa moja au siyo moja kwa moja wa kutoa msaada au rasilimali kwa mashirika au watu wanaojihusisha na ugaidi "ikiwamo mashirika yanayojihusisha na ugaidi kama ilivyofafanuliwa katika Ibara ya 102 ya Sheria ya Makosa ya Jinai na kamuni zilizoorodheshwa chini ya Sheria na Kanuni za Makosa ya Jinai zilizotokana na Sheria ya Mkataba wa UN; na
    b. Sheria na kanuni zinazohusiana na vitendo vya rushwa hususani hongo kwa maofisa wa nchini na nje ya nchi.
4. So They Can kwa kutambua halitalipa fedha zozote kwa mhalifu na mashirika au watu wanaojulikana au kushukiwa wanajihusisha na ugaidi.
5. So They Can litatoa taarifa kuhusu kosa lolote linalojulikana au kushukiwa kuwa la uhalifu au ugaidi au kuiwasilisha kwa mamlaka za nchi inayohusika.
6. So They Can litafanya jitihada zote kuhakikisha kwamba wapokeaji wote wa fedha za SoThey Can wanatumia sera na taratibu zinazowawezesha kufuata sheria ya Australia inayohusika na kupinga ugaidi na kuzuia uhalifu.
7. So They Can litahakikisha kwamba wafanyakazi wake, wale wanaojitolea na wahusika wa vyombo vya usimamizi wanapata mafunzo kuhusu athari za vitendo visivyoruhusiwa katika masuala ya fedha, kuzuia na kuripoti kama sehemu ya mafunzo ya uelekezi na kisha watawapatia mafunzo ya kuwapiga msasa kila mwaka.
8. So They Can litahakikisha kwamba Wawakilishi wake wote wanaelewa wajibu wao wa kuripoti bila kuchelewa masuala yoyote ya jaribio, shutuma, watashuku au kugundua shughuli za kihalifu au mtandao wa mashrika au watu wanaojihusisha na ugaidi. Masuala yoyote ya udanganyifu na rushwa yatashughulikiwa kwa siri, kwa haraka na kwa utaalamu wa kiwango cha juu kwa mujibu wa taratibu zilizobainishwa katika Sera ya Malalamiko ya SO They Can na Sera ya Watoa Taarifa za Uhalifu ya So They Can.

**TARATIBU**

1. So They Can litahakiki na kuweka rekodi za wafanyakazi wake, wajumbe wa bodi, wasambazaji na Wawakilishi wengine ili kuhakikisha kwamba hawasaidii au kuwa na uhusiano na magaidi au mashirika ya ugaidi yaliyobainishwa (yale yaliyo katika Orodha ya Jumla au Orodha ya Mashirika yanayojihusisha na Ugaidi) Wawakilishi wanapaswa kujua utambulisho, sifa na mwenendo mzuri wa washirika wao na

mashirika yanayopokea msaada (yaani wanafanya nini, wanafanyia wapi shughuli zao, wafanya uamuzi wao wakuu na wafanya kazi wao ni akina nani" .

2. Kabla ya kufanya kazi na mfanyakazi yeyote, mjumbe wa bodi, mtu anayejitolea na mwenye mkataba So They Can linatakiwa kufanya uhakiki kikamilifu wa Rekodi za Polisi wa Australiani kuhusu makosa ya jinai, au kuhakiki rekodi za Makosa ya Jinai katika nchi yoyote ambayo wanaishi au ambayo wameishi zaidi ya miezi kumi na miwili katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Wakati wa kipindi chote cha kufanya kazi na So They Can Uhakiki wa Makosa ya Jinai unapaswa kufanyika kila baada ya miaka miwili.
3. Uteuzi wa wafanyakazi wote utakamilika kutokana na taarifa nzuri zitakazotokana na uhakiki
4. Kabla ya uteuzi wa Mhusika (bodi ya wakurugenzi au wadhamini) So They Can itahakikisha hawakosi sifa za:
    - usimamizi wa kampuni chini ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2001(Cth) (Sheria ya Makampuni), au
    - kuwa Mhusika katika Kamishina ya ACNC, ndani ya kipindi cha miezi 12 iliyopita.

    kwa:

    - kumtafuta mtu huyo katika Rejista ya AISC ya Watu wasio na Sifa (ASIC Disqualified Persons Register)
    - kumtafuta mtu huyo Rejista ya ACNC ya Watu wasio na Sifa (ACNC Register of Disqualified Persons) (katika kipindi hiki ANC haijamuondoloe mtu yeyote sifa), na
    - kumtaka kila Mhusika Mkuu kusaini tamko (**Kiambatisho A**) linalothibitisha kwamba hawajaondolewa sifa na kwamba anaelewa nini maana ya kukosa sifa.
5. Kabla ya kusaini mkataba wa ushirikiano, Mkataba wa Maridhiano au wa Ufadhili, So They Can litahakikisha kwamba mashirika washirika na wawakilishi wao hawasaidii au kuhusiana na magaidi au mashirika yanayojihusisha na ugaidi yaliyobainishwa (yaani orodha ya magaidi na mashirika yanayojihusisha na ugaidi yaliyoorodheshwa na Serikali ya Australia, UN, Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo Asia)
6. So They Can itahamisha fedha kwa kutumia benki na taasisi nyingine zenye sifa tu kwa madhumuni haya na kwa kuzingatia taratibu zilizobainishwa katika Kanuni za Fedha za So They Can na Sera ya So They Can ya Uhamishaji Fedha Kimataifa.
7. Taratibu za kuzuia ugaidi zitajumuishwa katika sehemu ya Udhibiti wa Vihatarishi kwenye kila nyaraka ya kila nchi ya Mpango wa Mradi.
8. Kwa kadri inavyowezekana, washirika wote wa miradi ya So They Can watafahamishwa kuhusu wajibu wa So They Can chini ya sheria ya Australia na kuwajibika kufuata sheria kwa fedha zinazotoka katika vyanzo vya fedha za Australia.
9. Maombi ya So They Can na washirika wake yenye taratibu za mahesabu zinazokubalika kimataifa yanafanyiwa ukaguzi huru mara kwa mara.
10. So They Can litasitisha msaada wote haraka iwezekanavyo ikijumuisha utoaji wa rasilimali kama itakuwa na sababu ya kuamini kwamba wizara au washirika wa mradi wamekiuka masharti ya sera hii.
11. Kwa kadri inavyowezekana Mkataba wowote wa Maridhiano, ubia au ufadhili utajumuisha maneno yanayoyataka mashirika yanayopokea msaada kuzingatia sera na taratibu zinazoendana na masharti ya Serikali ya Australia. Maneno yanayopendekezwa na DFAT ni:

    "Shirika linatambua kwamba Serikali ya Australia inatumia sera na sheria zinazoendana na Mikataba ya Kimataifa ya kuzuia ugaidi na Azimio namba 1373 (2000) la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa la kutotoa msaada wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja au rasilimali kwa mashirika au watu

wanaojihusisha na ugaidi.

Shirika linapaswa kuchukua hatua stahiki kuhakikisha kwamba fedha zinazotolewa chini ya Mkataba huu zinatumika kwa namna inayozingatia Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na sheria za Australia zinazohusika. Ikitokea wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu, Shirika litabaini uhusiano wa aina yoyote ile na shirika lolote au mtu anayejihusisha na ugaidi linapaswa kuwajulisha haraka Polisi wa Shirikisho la Australia na/au AusAID. So They Can litafanya ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara kwa shughuli za miradi na program ili kuhakikisha fedha zinatumika kwa madhumuni yaliyokubaliwa na yaliyoidhinishwa. Wanaopokea fedha wanatakiwa kuwasilisha taarifa ya mahesabu kwa kila robo mwaka inayoonyesha namna fedha zilivyotumika.

12. Ikiwa mashirika au watu wanaopokea msaada watabainika kuwa katika orodha yoyote, fedha zinazotolewa zitasitishwa na taarifa itatolewa haraka kwa kupiga simu usalama wa taifa kwa namba 1800 123 400 (au namba +61 1300 123 401 kama simu inapigwa kutoka nje ya Australia).
13. So They Can litatoa taarifa kuhusu shughuli zozote zinazoshukiwa kuwa za ugaidi au uhalifu au kuhusiana na fedha za DFAT kwa DFAT ndani ya siku tano za kazi baada ya kubaini counter-terrorism.resourcing@dfat.gov.au.

**NYARAKA ZINAZOHUSIKA**

- Sera na Mwongozo wa Usajili wa So They Can
- Mwongozo wa Fedha wa So They Can
- Sera ya Uhamishaji Fedha Kimataifa ya So They Can
- Sera ya Ajira ya So They Can
- Sera ya Udanganyifu na Kuzuia Rushwa ya So They Can
- Sera ya Kutoa Taarifa ya So They Can
- Sera ya Malalamiko ya So They Can
- Mipango ya Miradi ya So They Can

| Tarehe | Toleo | Utekelezaji |
|---|---|---|
| 27 Februari 2019 | 1.1 | Urekebishaji wa sera kulingana na masharti ya DFAT |
| 15 Februari 2021 | 2.0 | Kubadilisha jina la Uhalifu wa masuala ya Kifedha<br><br>Sera ya Utakatishaji Fedha na Kuzuia Ugaidi |

| | | |
|---|---|---|
| | | Kuongeza shughuli za utakatishaji fedha na uhalifu katika yaliyomo katika sera |
| Mei 2021 | 2.1 | Ongezeko la taratibu za uhakiki<br><br>Jedwali la tamko la Wahusika wa kushughulikia Usajili wa watu wasio na sifa wa ACNC na ASIC limeongezwa. |

**KIAMBATISHO A**

## Tamko kwa Wahusika kuthibitisha kwamba hawajaondolewa sifa chini ya Kiwango cha 4 Usimamizi cha ACNC

Mimi, [jina] ……

wa[anwani] ……

……

……,

Ninathibitisha kwamba:

- Sijaondolewa sifa ya kusimamia kampuni, chini ya maana ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2001 (Cth) na
- Sijaondolewa sifa na Kamisheni ya Australia ya Msaada na Isiyo ya Kutengeneza Faida wakati wowote katika kipindi cha miaka ya nyuma kwa kutokuwa mwajibikaji (inayojulikana katika Sheria ya ACNC kama "taasisi inayohusika"

Wakati nikiwa Mhusika Mkuu wa (jina la msaada), Ninakubali kutoa taarifa haraka iwezekanavyo kama nitaondolewa sifa ya kusimamia kampuni kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni ya mwaka 2001, au kama nitaondolewa sifa na Kamishina wa Mashirika ya Msaada na Yasiyotengeneza Faida ya Australia. Wahusika ni wajumbe wa vyombo vya usimamizi wa msaada ambao wana jukumu la kusimamia msaada (wanaoitwa vyombo vinavyohusika chini ya Sheria ya ACNC)

Tamko limetolewa: [eneo]

……

Tarehe:

……

Saini:

……

Jina:

……

Cheo:

……